

Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | March-2026

EAJK

# Uchanganuzi wa Majina ya Wanaume Katika Jamii ya Watugen

**Authors**

**Dave Bowen**

**Author's email:** tbowenza001@gmail.com

**Kabarak University, Kenya.**

**Cite this article in APA**

Bowen, D. (2026). Uchanganuzi wa majina ya wanaume katika jamii ya Watugen. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 5*(1), 24-31. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.887

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-01-17
Accepted: 2026-02-14
Published: 2026-03-18

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Utafiti huu ulichambua majina ya wanaume katika jamii ya Watugen, Kaunti ya Baringo ya Kati, Kenya. Lengo kuu lilikuwa kuchunguza majina haya miongoni mwa wanajamii wa eneo hilo. Ingawa majina ya kipekee katika jamii hii hujumuisha yale yanayotokana na mito, milima, vijiji, miji, watu na nchi, uchunguzi ulijikita kwenye majina ya wanaume pekee. Makala hii inajumuisha vijisehemu vifuatavyo: maelezo mafupi kuhusu jamii ya Watugen, utamaduni wa kupeana majina, sherehe zinazohusiana na kupeana majina, majina ya wanaume pamoja na maana zao, na hitimisho. Utafiti uliongozwa na nadharia ya simiotiki, ambayo inasisitiza kuwa kila ishara ina maana yake maalum. Data zilikusanywa kwa njia ya uchunguzi wa nyanjani kwa kutumia mbinu ya mahojiano. Washiriki 50, ambao walikuwa watu wazima wenye umri kati ya miaka 35 na 70, walihojiwa kwa muda wa majuma mawili. Sampuli ya majina iliorodheshwa katika majedwali ili kuwezesha uchambuzi. Utafiti uliongozwa na maswali yanayohusu Watugen ni watu wa wapi, sherehe zipi zilihusiana na kupeana majina, sababu za ujinaishaji zilikuwa zipi, kategoria zipi za majina zilikuwepo, na maana za majina ya wanaume zilikuwa zipi. Majibu ya maswali haya yaliunda kiini cha utafiti. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa majina ya wanaume yalitokana na hali halisi za kijamii katika jamii ya Watugen, na kila jina likibeba maana maalum. Ilibainika kuwa ujio wa wageni, hasa wamishonari, uliathiri sana mchakato wa ujinaishaji. Zaidi ya hayo, majina hayo yana miundo mbalimbali.

**Maneno muhimu:** Jamii na simiotiki, maana ya majina, majina ya wanaume, sherehe za kupeana majina.

**UTANGULIZI**

Jamii ya Tugen imo katika eneo la Kaunti ya Baringo nchini Kenya, Afrika Mashariki. Kaunti ya Baringo ina kaunti ndogo zifuatazo: Mogotio, Eldama Ravine, Tiaty, Baringo ya Kati, na Baringo Kaskazini.Lugha ya Kitugen ndiyo lugha kuu inayotumiwa katika takriban kaunti ndogo zote za Kaunti ya Baringo. Hata hivyo, kuna watu wanaoongea lugha za kigeni, hasa katika miji mikuu kama Kabarnet, Eldama Ravine, na Mogotio. Katika maeneo hayo, Kiswahili hutumika kama lugha ya mawasiliano. Kiswahili ni lugha unganishi katika Kaunti ya Baringo kwa ujumla.

Kaunti ya Baringo ina lahaja zifuatazo za lugha ya Kitugen: Samor (Baringo ya Kati), Lembus (Eldama Ravine/Koibatek), Keben (Baringo Mashariki), Aror (Baringo Kaskazini), na Pokot (Baringo Mashariki) (Towett, 1979; Ogot, 1967; Chesaina, 1991). Lahaja hizi zote ni michomoko ya lugha moja, yaani Kitugen, kwa sababu wazungumzaji wa lahaja hizo huweza kuwasiliana kwa urahisi na wana mambo mengi yanayoingiliana, kama vile mila sawa, historia moja, na imani zinazofanana. Kila jamii ya lahaja husika ina mbari au milango tofauti.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Utamaduni wa Majina**

Wataalamu wa onomastiki wanasema kuwa utamaduni wa majina katika jamii mbalimbali hutokea katika muktadha wa utamaduni maalum (Herbert, 1995). Kwa mujibu wa Herbert (1995) kama alivyonukuliwa na Leyew (2003), utafiti wa onomastiki unahitaji kulenga masuala ya isimujamii, ambayo yanajumuisha: Mtoto ni nani? Mtoto hupewa jina lini? Jina huteuliwa vipi? Mtoto hupewa jina hadharani au faraghani? Jina hubuniwa au hutolewa kutoka majina yaliyopo katika jamii?

Jamii ya Tugen, kama jamii nyingine za Kiafrika, ilitilia maanani sherehe za ujinaishaji bila kujali jinsia ya mtoto. Maoni haya yanashabiana na yale ya Crane (1982), ambaye alisema kuwa majina ya watu yaliheshimiwa sana na kuchukuliwa kama milki muhimu ya binadamu. Watu walimiliki majina yao hata baada ya kifo. Majina mengi hutekeleza majukumu zaidi ya kutambulisha mtu tu; huwa na maana mahususi yanayohusiana na hali ya kisiasa, kiuchumi au kijamii. Katika jamii ya Tugen, kama jamii nyingine za Kiafrika, majina huwa wazi na husheheni maana. Kila jina la mwanamume lilikuwa na maana maalum, na mara nyingi lilihusishwa na tukio muhimu katika jamii (Tuitoek, 2010). Jamii ya Tugen ilikuwa na kategoria mbalimbali zilizoelekeza ujinaishaji, kama vile muktadha wa kuzaliwa, wakati wa kuzaliwa, tabia za mtoto, matatizo ya uzazi katika familia fulani, na mengineyo.

**Utamaduni wa Sherehe za Ujinaishaji**

Sherehe za kumpa mtoto wa kiume jina ni sawa na zile za mtoto wa kike. Tuitoek (2010) anasema kuwa sherehe ya kumpa mtoto jina miongoni mwa Watugen ilijulikana kama *Lugumian*. Mtoto hakupewa jina mara tu alipozaliwa; mchakato ulianza siku chache baada ya mama kujifungua. Wazazi wa mtoto ndio waliopewa jukumu la kuchagua jina, lakini walitakiwa kutafuta ushauri kutoka kwa wanajamii wengine wa ukoo, kama babu, nyanya na shangazi. Kwa hivyo, sherehe ilianza na wazazi kushauriana na babu na nyanya, ambao walistahiki heshima kubwa katika jamii. Jamii iliamini kuwa wazee ndio walioelewa vizuri masuala ya koo au nasaba.

Siku ya ushauri, wazazi walilazimika kuwapa babu au nyanya kibuyu cha busaa (au *komek*). Babu au nyanya walimpa mtoto jina kulingana na jinsia yake. Baada ya majuma mawili, kina mama majirani walizuru boma la mtoto ili kuthibitisha jina lililopeanwa na babu au nyanya. Kina mama hao walichukuliwa kuwa sehemu ya sherehe rasmi ya ujinaishaji.

Wakati wa sherehe kuu ya kumpa mtoto jina, mbali na kina mama, watoto wote wenye umri chini ya miaka saba kutoka familia jirani walialikwa. Kina mama walithibitisha jina kwa vigelegele na vifijo, na tangazo hilo lilijulikana kama *Keostoji kainet*. Siku hiyo ilikuwa muhimu sana kwa mtoto aliyezaliwa. Watoto waalikwa waliingia nyumbani kwa vifijo na nderemo kama ishara ya kuadhimisha kuzaliwa kwake na hafla ya kupewa jina. Nyimbo iliyotumiwa ilijulikana kama *Ang tolagat kou ra angot anee, ang tolagat kou*, na ilirudiwa mara kwa mara. Baadaye, watoto waliketi kwa mviringo na kupakuliwa ugali wa wimbi bila kitoweo cha mboga au maziwa. Walikula chakula hicho wakiwa wamenyamaza kama ishara ya kumkaribisha mtoto katika kundi lao. Mtoto alitarajiwa kufahamu jina lake baadaye, ingawa hakutarajiwa kulitaja kwa sauti, kwani hilo lilikuwa mwiko. Sherehe ya kumpa mtoto

jina ilikuwa muhimu kwa wazazi pia (Madubuike, 1994).

**Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya semiotiki. Halliday (1978) anaeleza kuwa semiotiki ni dhana inayotokana na neno la Kigiriki *semainon au semainomenon*, ambalo linamaanisha "kiashiria" na "kiashiriwa". Semiotiki ni taaluma inayochunguza ishara na maana zake (Wamitila, 2003). Zaidi ya hayo, semiotiki inahusu jinsi maana inavyotokana na ishara katika muktadha wa kijamii. Nadharia hii inamwezesha binadamu kutazama vitu na hali mbalimbali kama ishara zenye maana maalum (Wafula & Njogu, 2007).

Waasisi wakuu wa nadharia ya semiotiki ni mwanaisimu Ferdinand de Saussure (1857–1913), ambaye alihusishwa na nadharia ya umuundo, na mwanafalsafa Charles Sanders Peirce (1839–1914). Saussure alisisitiza umuhimu wa ishara katika jamii, huku Peirce akichunguza jinsi ishara zinavyohusiana na mantiki ili ziwe na maana. Saussure alisisitiza kuwa ishara ina pande mbili: kiashiria na kiashiriwa. Kiashiria ni umbo linaloweza kuonekana, kusikika, kunuswa au kuonjwa, wakati kiashiriwa ni dhana au maana inayotokana na kiashiria. Kwa hivyo, kiashiria na kiashiriwa huhusiana. Ishara hutumiwa kueleza vitendo mahususi katika lugha maalum, na watu fulani hutumia ishara hizo kuelewa na kuwasiliana (Scholes, 1974).

Nadharia ya semiotiki inafaa sana katika kuelewa namna ya kufasiri maana ya majina ya wanaume katika jamii ya Tugen. Majina ya watu yanategemea utamaduni na muktadha wa jamii husika. Katika utafiti huu, majina ya wanaume huwa na maana maalum ambayo inapatikana kwa kutazama ishara kama mfumo mzima badala ya kuangalia jina peke yake.

**MBINU ZA UTAFITI**

Data zilikusanywa kutoka kwa wakaazi wa Kaunti ya Baringo wanaoongea lugha ya Kitugen kama lugha yao ya kwanza. Mbinu ya mahojiano ilitumika kukusanya data kutoka kwa washiriki 50, ambao walikuwa watu wazima wenye umri kati ya miaka 35 na 70. Mahojiano yalifanyika kwa muda wa majuma mawili. Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa ili kuwateua washiriki wa utafiti huu, Pamoja na hayo, maandishi kuhusu utamaduni na historia ya Watugen ilipitiwa. Data zilizokunsanywa zilichanganuliwa kwa msingi wa nadharia ya Semiotiki.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa majina ya wanaume katika jamii ya Tugen yalikuwa na maana maalum kwa mwenye jina. Kiutamaduni wavulana walipewa majina mawili, na kila jina lilikuwa na maana fulani kwa mtoto, familia na jamii. Jina la kwanza liliashiria jinsia ya mtoto. Jina la kwanza la mtoto lilijulikana kama *Kainetab musarek.*

Mtoto alipewa jina la pili kutegemea wakati mtoto alizaliwa; mchana au usiku. Kwa mfano, Watoto wengine walipewa majina kutegemea shughuli za wakati walipozaliwa, majira au misimu na wengine wakapewa majina ya Wanyama kwa sababu ya mikosi katika familia husika. Majina ya wanaume katika jamii ya Tugen yanajitokeza kwa makundi yafuatayo:

**Majina Yanayotokana na Nyakati**

Jamii ya Tugen iliwapa watoto majina kutegemea wakati wa kuzaliwa kwao. Watoto wavulana walipewa majina yanayotangulia na kiambishi {ki} halafu kiini cha jina lenyewe ambacho hubeba maana ya jina. Majina haya ya wakati huashiria wakati maalum ya siku. Mtoto anaweza akazaliwa usiku au mchana hata hivyo, wakati huenda usiwe maalum. Nyakati zinaweza kuwa kwa jumla tu kama vile asubuhi na mapema, mchana au usiku bila kutaja wakati mahususi.

**Jedwali 1 : Majina Yanayotokana na Nyakati**

| JINA | Maana |
|---|---|
| *Kibet.* | Mtoto aliyezaliwa mchana |
| *Kiplagat.* | Mtoto aliyezaliwa usiku |
| *Kipkorir.* | Mtoto aliyezaliwa alfajiri |
| *Kipkoech.* | Mtoto aliyezaliwa mapambazuko |

Kutokana na jedwali ni bayana kwamba Watoto wa kiume walipewa majina yenye kiambishi {ki} na hufuatwa na mizizi yenye miundo tofauti tofauti. Kiambishi {ki} kiliashiria jinsia ya kiume. Mizizi ya majina huishia kwa aidha vokali au konsonanti yoyote ile kwa mfano, katika majina yaliyomo kwenye jedwali, majina hayo yameishia kwa konsonanti t, r na ch.

**Majina Yanayotokana na Mahali pa Kuzaliwa**

Jamii nyingi za Kiafrika hutumia mbinu ya mahali pa kuzaliwa kuwapa majina Watoto (Sitati, 2007). Kwa hivyo, mahali pa kuzaliwa mtoto ni muhimu katika kuwapa majina watoto miongoni mwa wanajamii katika jamii ya Tugen. Mbinu hii ilitumiwa kuwapa wavulana majina ya kipekee.

**Jedwali 2: Majina Yanayotokana na Mahali pa Kuzaliwa**

| Jina | Maana |
|---|---|
| *Kibor/Chebor* | Mtoto aliyezaliwa kwenye njia. |
| *Kibii/Chebii* | Mtoto aliyezaliwa kwa zizi la ng'ombe. |
| *Kipsang/Chesang* | Mtoto aliyezaliwa nje ya nyumba. |
| Kipserem/Cheserem | Mtoto aliyezaliwa kwenye /boma. |
| *Kiptarus/Cheptarus* | Mtoto aliyezaliwa unyagoni. |

Kutokana na mifano kwenye jedwali inadhihirika kwamba majina ya wanaume kutokana na mahali walipozaliwa huchukua vianzio viwili: {che}, {Chep} au {kip}, vianzio hivyo vya majina hufutwa na jina la mahali mtoto alizaliwa. Kwa mfano nomino ya kawaida *Bii* hujalizwa kiambishi {ki} na kuwa jina la kipekee cha mtoto wa iume na kuwa *Kibii* au *Chebii*. Katika utamaduni wa Tugen, mvulana hupewa jina linaloanza kwa kiambishi {kip} lakini baada ya kupashwa tohara muundo wa jina hubadilika na kuchukua kiambishi {che} kuashiria kwamba yeye amepandishwa hadhi na kuwa mwanaume katika jamii.

Majina haya yanadhihirisha mahali maalun ambapo mtoto wa kiume alizaliwa kwa mfano, njiani, chini ya mti, ghalani au bustanini. Kwa hivyo, majina haya yalidhihirisha mahali ambapo mtoto alizaliwa.

**Majina Yanayotokana na Matukio Mbalimbali**

Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kwamba baadhi ya majina ya wanaume yalitokana na majina ya matukio yaliyojiri wakati walipokuwa wakizaliwa. Matukio muhimu katika jamii yalitumiwa kuwapa Watoto wa kiume majina. Mbinu hii ya kuwapa majina Watoto ilikuwa maarufu katika jamii za Kiafrika (Kimenyi, 1978). Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi ya majina yanayotokana na matukio mbalimbali katika jamii ya Watugen.

**Jedwali 3: Majina Yanayotokana na Matukio Mbalimbali**

| Jina | Maana |
|---|---|
| *Kiptoo/Cheptoo* | Mtoto aliyezaliwa wakati wageni walipozuru kwao. |
| *Kiprop/Cherop* | Mtoto aliyezaliwa msimu wa mvua. |
| *Kipruto/Cheruto* | Mtoto aliyezaliwa wakati wa kutembelewa. au matembezini. |
| *Tuitoek* | Mtoto aliyezaliwa wakati wageni wanapokutana. |
| *Toroitich* | Mtoto aliyezaliwa wakati kukaribisha ng'ombe wanaporejea nyumbani kutoka malishoni. |
| *Barwesa* | Kuashiria aidha, tukio la mauaji yalitokea mtoto akizaliwa au mmlika wa jina aliua. |
| *Bargoret* | Kuashiria aidha, tukio la mauaji yalitokea mtoto akizaliwa au mmlika wa jina aliua. |
| *Bartonjo* | Kuashiria aidha, tukio la mauaji yalitokea mtoto akizaliwa au mmlika wa jina aliua. |

Kutokana na mifano kwenye jedwali, inadhihirika kwamba majina wa wanaume kutokana na matukio katika jamii huchukua vianzio vitatu: {che}, {Chep, {Bar} au {kip} au {ϴ}, vianzio hivyo vya majina hufuatwa na jina la matukio yaliyotokea mtoto alipozaliwa. Kwa mfano nomino ya kawaida *Rop* hujalizwa kiambishi {ki} na kuwa jina la kipekee cha mtoto wa kiume na kuwa *Kipropi* au *Cherop*. Aidha, majina mengine hujitokeza bila viambishi {che}, {Bar}, {Chep} au {kip} lakini hutanguliwa na vitenzi vya matukio yanayohusika. Hujitokeza kama majina ambatani kutoakana na kitenzi na nomino. Kwa mfano, kitenzi {*tui*}-kutana huambishwa na nomino ya kawaida {toek}- wageni, yaani wingi wa toyot(mgeni) kutokana na muundo wa kiisimu wa lugha ya tugen pale ambapo sentensi hutangulia na kitenzi yaani T+N. Katika utamaduni wa Tugen, mvulana hupewa jina linaloanza kwa kiambishi {kip} lakini baada ya kupashwa tohara muundo wa jina hubadilika na kuchukua kiambishi {che} kuashiria kwamba yeye amepandishwa hadhi na kuwa mwanaume katika jamii.

**Majina Yanayotokana na Tabia au Sifa za Kimaumbile**

Jamii ya Watugen iliwapa majina Watoto wa kike kwa msingi wa tabia au sifa zao, kwa mfano, msumbufu, mweusi, mweupe, mdogo au mnyenyekevu na kadhalika. Haya yalitegemea maumbile ya mtoto, mara nyingi majina kama haya yalitokana na vivumishi mbalimbali vya mtoto (Mwangi, 2017).

**Jedwali 4: Majina Yanayotokana na Tabia au Sifa za Kimaumbile**

| **Jina** | **Maana** |
|---|---|
| *Kiptui* | Mtoto aliyezaliwa na sura nyeusi. |
| *Kiptai/Cheptai* | Mtoto aliyezaliwa wa kwanza. |
| *Toweet* | Mtoto aliyezaliwa mwisho (Kitindamimba). |
| *Kimaru* | Mtoto aliyezaliwa asiyelala kila wakati. |
| *Kiptanui* | Mtoto anayezirai kila wakati. |
| *Kibichii* | Mtoto msumbufu. |

Kutokana na majina haya, tunapata kuzielewa sifa za Watoto wanaomiliki majina hayo. Tabia hizo zilidhihirishwa walipokuwa Watoto wachanga. Hata hivyo, baadhi ya sifa hizo zilisalia hadi utu uzima, kwa mfano sura zao hasa rangi za miili yao. Mtoto akizaliwa mweusi atasalia vivyo hivyo hata atakapokuwa mtu mzima.

**Majina Yanayotokana na Mtoto 'Kukataa' Kuzaliwa Hadi Jamaa Zao Fulani Wafike**

To huenda mama akakawia sana kujifungua nahalafu anajifungua punde tu jamaa zao fulani wanapowasili kwa mfano, shangazi, mjomba, au nyanya au babu.

**Jedwali 5: Majina Yanayotokana na Mtoto 'Kukataa' Kuzaliwa Hadi Jamaa Zao Fulani Wafike**

| **Jina** | **Maana** |
|---|---|
| *Kanygogo.* | Mtoto anayezaliwa punde tu nyanya anapowasili. |
| *Kanykwony* | Mtoto aliyezaliwa punde mama fulani anapowasili. |
| *Kanymama.* | Mtoto aliyezaliwa punde tu mjomba anapowasili. |

**Majina Yanayotokana na Mtoto Kuzaliwa Bila Usaidizi wa Mkunga**

Watoto ambao walizaliwa bila usaidizi wa wakunga walipewa majina maalum. Mama akifanikiwa kujifungua peke yake bila usaidizi wa mkunga basi mtoto hupewa jina maalum kuashiria tukio hilo. Majina kama hayo yalipatikana katika jamii ya Watugen zamani na hali bado ni hiyo hata wakati huu. Baadhi ya majina kama hayo yameorodheshwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali 6: Majina Yanayotokana na Mtoto Kuzaliwa Bila Usaidizi wa Mkunga**

| Jina | Maana |
|---|---|
| *Kipleting* | Mtoto aliyezaliwa bila usaidizi wa mkunga |
| *Kipsige* | Mtoto aliyezaliwa bila usaidizi wa mkunga |
| *Kipsuge* | Mtoto aliyezaliwa bila usaidizi wa mkunga |

**Majina Yanayotokana na Wanyama Mbalimbali**

Jamii ya Watugen ilikuwa na majina ya Watoto wa kiume yaliyoashiria mambo mbalimbali. Kwa mfano, kurejelea wanandoa waliokuwa na changamoto kuzaa watoto kwa muda mrefu sana au wanandoa wanaopata shida kuavya mimba mara nyingi. Watoto kama hawa walipewa mjina la kitasfida *Tegerin* au *Tegerion.* Mara nyingi majina hayo yalitokana na Wanyama wanaoaminika kuleta mikosi katika jamii. Lengo lilikuwa kuwalinda Watoto dhidi ya pepo wabaya katika jamii. Baadhi ya majina hayo yalikuwa kama yalivyoorodheshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 7: Majina Yanayotokana na Wanyama Mbalimbali**

| Jina | Maana |
|---|---|
| *Kipberen/Cheberen* | Nyoka. |
| *Kipkuto/Chepkuto* | Ant eater. |
| *Kipmoso/Chemoso* | Nyani |
| *Kimelilil/Chemelil* | Chui. |
| *Cheboi* | Pepo Wabaya. |
| *Kugui* | Mamba. |

**Majina Yanayotokana na Matukio ya Majanga Mbalimbali**

Majina yalitokana na majanga yaliyoyoyukia katika historia jamii ya Watugen. Majina kama haya katika jamii hutumika kama nyaraka zenye uamilifu wa kuweka rekodi za matukio hayo (Mwangi, 2017). Matukio ya majanga haya yalihusu; ukame, njaa, uvamizi wa nzige, mikurupuko wa magonjwa na kadhalika

**Jedwali 8: Majina Yanayotokana na Matukio ya Majanga Mbalimbali**

| Jina | Maana |
|---|---|
| *Kiptalam/Tallam* | Nzige |
| *Kipkemei/Chepkemei* | Ukame? Njaa |

Majina haya yanatuelekeza kwa historia ya jamii ya watugen kwa upande wa matukio ya majanga. Matumizi ya matukio ya majanga kuwapa Watoto majina yalijitokeza katika jamii nyingi za Kiafrika. Haya yanadhirisha kwamba jamii nyingi zilikumbwa na majanga haya. Uvamizi wa nzige umetanda katika jamii nyingi kwa mfano, jamii ya wakikuyu wan nchi ya Kenya, jina *Ngige* (Kiume) na miongoni mwa jamii ya Wabukusu *Wasike* (kiume) hurejelea uvamizi wa nzige.

**Majina Yanayotokana na Ukoo wa Mama**

Majina ya koo yanaweza kutumiwa kama majina ya watu katika jamii (Rubanza, 2000). Ijapokuwa jamii ya Wtugen ilitawaliwa na wanaume, wanawake walikubaliwa kumilika majina ya koo zao hata baada ya kuolewa kwa ukoo tofauti. Jamii ya Watugen ilikuwa na koo nyingi. Kwa hivyo, wanawake wengi waliendelea kutumia majina ya koo zao. Kwa mfano, *Tungo, Kimoi, Targog, Toyoi, Kabilo, Sote, Sogoom* na kadhalika. Majina haya ya ukoo yalitumiwa kuwapa majina vitindamimba wa kiume. Katika jamii ya Watugen, iliaminika kwamba mtoto wa kiume kitinda mimba alikuwa ni wa mama n ahata alitikwa jukumu kumtunza mama alipozeeka n ahata kurithi mali ya mama yake. Baada ya kupaswa tohara, mtoto wa kiume kitindamimba alipewa jina hilo la ukoo na jina *Arap* lilijalizwa kabla ya jina la ukoo wa mama, kama vile *Arap Tungo kutokana na* Ukoo wa *Tungo*. Baadhi ya majina hayo yalikuwa kama yafuatayo:

**Jedwali 9: Majina Yanayotokana na Ukoo wa Mama**

| **Jina** | **Jina la Ukoo** |
|---|---|
| *Arap Tungo* | *Tungo* |
| *Arap Targog* | *Targog* |
| *Arap Kabilo* | *Kabilo* |
| *Arap Kimoi* | *Kimoi* |
| *Arap Sote* | *Sote* |
| *Arap Kimoi* | *Kimoi* |

**Majina kutoka Lugha za Kigeni**

Majina mapya yaliingizwa katika jamii ya kitugen kutokana na maajilio ya wazungu na mtagusano wao na wenyeji. Wazungu wa kwanza kuingia eneo la Baringo walikuwa wakoloni na wamisionari. Wamisionari walifika mnamo mwaka wa 1907 na wakawa na makao yao katika mji wa Eldama Ravine kabla ya kusambaza athari zao kwa maeneo kama Emining, Kapropita na Kabartonjo (Tutoek, 2020). Hata hivyo, wamisionari waleta athari kubwa kwa ujinaishaji wa wenyeji hasa wale ambao walipokea dini ya Kikristo. Mwanzoni, baada ya kuokoka na kufuata imani ya Kikristo na kubatizwa wavulana walipewa majina kutoka Biblia. Lakini baadaye jamii nzima ilifuata utamaduni wa kuwapa wavulana majina ya kidini na ya kigeni kwa jumla hususan baada ya kupaswa tohara, majina kama haya yaliegemea uchaguzi wa wazazi wa wavulana. Utafiti huu ulidhihirisha kwamba majina ya kigeni yalitoholewa na kufanyiwa marekebisho kabla ya kuingizwa katika lugha ya Kitugen. Majina mengi yalichukua miendelezo ya lugha ya Kiswahili. Majina hayo yalitokana na tafsiri ya Biblia kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili na hatimaye lugha ya Kitugen.

Baadhi ya majina wanaume kutoka Biblia katika jamii ya Kitugen ni kama katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali 10: Majina kutoka Lugha za Kigeni**

| **Jina la Biblia** | **Jina katika lugha ya Kitugen** |
|---|---|
| *Mathew* | *Matayo* |
| *Moses* | *Musa* |
| *Mike* | *Mika* |
| *Caleb* | *Kaleb* |
| *Timothy* | *Timoteo* |

Kutokana na mifano ya majina katika jedwali ni dhahiri kwamba majina mengi ya wanaume yalitoka Biblia na majina hayo yalifanyiwa marekebisho ya kifonolojia na kimofolojia kabla ya kuingizwa katika lugha ya Kitugen. Majina hayo yalitumiwa Pamoja na majina ya kiasili kama majina ya kwanza kwa hivyo, watu wangekuwa na majina matatu, yaani, jina la kwanza la Kikristo, jina la pili la kiasili na kisha jina la baba au familia. Kwa mfano. *Joana kipng'etich Cheserem*.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Utafiti huu ulichambua majina ya wanaume katika jamii ya Watugen na kudhihirisha kuwa majina hayo mbalimbali huashiria maana maalum. Majina yalitokana na matukio, mahali pa kuzaliwa, tabia za mtoto na mengineyo. Majina hayo yalifuata mila na desturi za ujinaishaji katika jamii ya Watugen na yalibeba maana fulani katika muktadha wa kijamii. Majina mengine yalitokana na majina ya wanyama waliohusishwa na mikosi katika jamii au familia mahususi. Aidha, majina ya wanaume yalionyesha matukio ya kihistoria katika jamii ya Watugen. Majina hayo pia yanadhihirisha athari na mwingiliano wa jamii ya Watugen na jamii za kigeni, hasa Wazungu wakiwemo wamisionari. Majina ya kigeni yamechangia orodha ya majina katika jamii ya Watugen. Majina ya kwanza yalitokana na majina ya Biblia, ambayo yalifanyiwa marekebisho ya kifonolojia na kimofolojia kabla ya kuingizwa katika lugha ya Kitugen.

**MAREJELEO**


*Chesaina, C. (1991). Oral literature of the Kalenjin. East Africa Educational Publishers Ltd.*
*Crane, R. (1982). African names, people and places: Teaching manual.*
*Halliday, M. A. K. (1978). Language as social semiotic: The social interpretation of language and meaning. Edward Arnold.*
*Kimenyi, A. (1998). Aspects of naming in Kinyarwanda. Anthropological Linguistics, 20(6), 258–271.*
*Leyew, Z. (2003). Amharic personal nomenclature: A grammar and socio-cultural study. Journal of African Cultural Studies, 16(2), 181–211.*
*Madubuike, I. (1994). A handbook of African names. Three Continents Press.*
*Mwangi, P. (2017). Lugha na fasihi katika karne ya ishirini na moja. Moi University Press.*
*Ogot, B. A. (1967). Hadith II: Proceedings of the annual conference of the Historical Association of Kenya. East African Publishing House.*
*Peirce, C. S. (1991). Front matter. In J. Hoopes (Ed.), Peirce on signs: Writings on semiotic by Charles Sanders Peirce (pp. i–iv). University of North Carolina Press. http://www.jstor.org/stable/10.5149/9781469616810_hoopes.1*
*Scholes, R. (1974). Structuralism: An introduction. Yale University Press.*
*Seroney, K. (n.d.). Samburtaab Ng'aleekaab Kaleenchin: Kalenjin dictionary. Mvule Africa Publishers.*
*Sitati, W. (2007). Comprehensive names dictionary. SAS Enterprises.*
*Towett, T. (1979). A study of Kalenjin linguistics. Kenya Literature Bureau.*
*Tuitoek, K. (2010). The Tugen community. St. Mary's Printing Press*